

# Watu Mazingira

Ulimwenguni!

DISEMBA 31 2018
TOLEO 4

## Rasilimali Bahari

**Kitega Uchumi Muhimu Bara Afrika**

**Msitu Wa Madunguni**

*Msitu Asilia Wa Pwani Ya Kenya Unaoangamia Polepole.*

**Kilimo Hifadhi**

*Kinabadilisha Maisha Ya Wakazi Wa Kaunti Ya Kwale, Kenya.*

**Bustani Za Matumbawe**

*Mbinu Mbadala Ya Kuboresha Mazingira Ya Bahari.*



# Yaliyomo


**03** **MTAZAMO WA MWAKA**
Maelezo ya Jumla kuhusu Mtandao wa Watu Mazingira Ulimwenguni

**04** **KILIMO HIFADHI**
Kinabadilisha Maisha ya Wakazi wa Kaunti ya Kwale, Kenya

**06** **RASILIMALI BAHARI**
Kitega Uchumi Muhimu Bara Afrika kinachoweza kutimiza ndoto ya 'Africa Tunayoitaka'

**08** **BUSTANI ZA MATUMBAWE**
Mbinu mbadala ya Kuboresha Mazingira ya Bahari

**10** **MSITU WA MADUNGUNI**
Msitu Asili wa Pwani ya Kenya Unaoangamia Polepole

# Mtazamo Wa Mwaka

## Muktasari wa Ripoti ya 2018

Mtandao wetu wa Watu Mazingira Ulimwenguni umekuwa ukipanuka kwa haraka tangu 2017, wakati tulipobadilika kuwa vuguvugu la kimataifa. Wanachama wetu wamefika 424 kutoka nchi 16 ulimwenguni. Nchi hizi ni Bangladesh, Benin, Cameroon, Costa Rica, Ethiopia, Ghana, Kenya, Malagasi, Marekani, Msumbiji, Namibia, Nepali, Tanzania, Uganda, UJapani, na Zimbabwe.

Msukumo mkubwa mwaka wa 2017 ulikuwa kujenga mtandao wa kimataifa kwa kuunda vitengo mbalimbali kama vile Kamati Kuu na Jukwaa saba za majadiliano. Lakini 2018, juhudi za mtandao zilielekezwa kwa kusajili wanachama na kuhakikisha vitengo mbalimbali vinafanya kazi ipasavyo.

Shughuli za Jukwaa zetu zilikuwa ni mijadala na usambazaji habari kupitia mitandao ya kijamii. Mijadala mingi ilihusu mikakati muafaka ya kuendesha na kutekeleza kazi za Jukwaa husika. Hatimaye, kuna sera, mikakati na miongozo kadhaa ambayo ilipitiwa ama kuundwa. Sera ya Kulinda Watoto (Jukwaa la Vijana), Mkakati wa Mawasiliano (Jukwaa la Elimu na Hamasisho), Mkakati wa Upanzi wa Miti (Jukwaa la Wanyama Pori na Misitu) na Mkakati wa Hazina Mazingira (Jukwaa la Biashara Mazingira) ni baadhi ya sera na mikakati muhimu iliyoundwa.


Mpango wetu wa kuwekeza katika shughuli za kimazingira zimezidi kutupa mapato mazuri, ijapokuwa mwaka huu mapato yalienda chini ikilinganishwa na 2017.

Kioto cha Wasini hakikuwa na shughuli nyingi mwaka huu. Hata hivyo, mipango inakamilika ya kuanzisha upya shughuli za mradi ifikapo mwaka ujao (2019). Kwa wakati huu, Kioto cha Kawi Safi kwa Jamii kimeendelea kutoa huduma ya kuwapa jamii vifaa vya sola na majiko ya kisasa ya kuhifadhi kawi.

Mwaka huu, tumeweza kutoa toleo la jarida letu la Watu Mazingira Ulimwenguni. Toleo la kwanza lilitoka Machi 2018 na tumeweza kutoa toleo kila robo mwaka. Jarida zetu zimeweza kuwafikia wanachama wetu na wadau wengine kupitia kwa mitandao ya kijamii na barua pepe.

Tungependa kuwashukuru nyote kwa kutuwezesha kupata mafanikio haya kwa kuhusika kwenu katika shughuli mbalaimbali za mtandao wetu. Tungependa kuwashukuru zaidi hasa tunapotazamia kuhusika kwenu katika mafanikio zaidi mwaka ujao (2019).

Kwa habari zaidi, tazama Ripoti ya Watu Mazingira Ulimwenguni Mwaka 2018.




Report ya Mwaka 2018



Silvanus Uunona,
Mwenyekiti,
Watu Mazingira Ulimwenguni
(NAMIBIA).

# KILIMO HIFADHI

## Kinabadilisha Maisha Ya Wakazi  Wa Kaunti Ya Kwale, Kenya.

Mbinu nyingi za kilimo zinazotumika na wakulima zimefanya udongo kuisha rotuba na kutozalisha mazao mazuri. Udongo usio rotuba, pamoja na mabadiliko ya hali ya hewa ya mara kwa mara, umefanya wakulima kutoweza kuwa na mpangilio mzuri wa kukuza mimea kwa uzalishaji bora. Wakulima sasa wamegeukia kilimo hifadhi ili kudhibiti changamoto hizi.

Shirika la Chakula Duniani chini ya Umoja wa Mataifa, imefafanua kilimo hifadhi kuwa mfumo wa kilimo ambao unahakikisha kuwepo kwa funiko la udongo wakati wote, uchimbaji kidogo wa udongo na upanuzi wa mimea mbalimbali. Kilimo hifadhi kinalenga utoaji wa mazao bora, kupunguza gharama ya kilimo na kuhifadhi uwezo wa udongo kutoa mazao bora kila wakati.

Ni kwa sababu hii mataifa mengi yamegeukia kilimo hifadhi kama suluhu kwa uzalishaji duni wa udongo, na kuwezesha wakulima kumudu mabadiliko ya hali ya hewa.

Mwaka wa 2015, Serikali ya Kaunti ya Kwale iliingia katika mkataba na shirika la Chakula Duniani kwa minajili ya kutekeleza mradi wa kilimo hifadhi. Mradi huu ni moja wa mradi mkubwa wa Udhibiti wa Hali ya Hewa Kenya Kupitia Kilimo Bora. Mbali na Kaunti ya Kwale, mradi huu pia unapatikana Kaunti za Kilifi, Taita Taveta, Makueni, Embu, Laikipia, Meru, Kitui, Machakos, na Tharaka Nithi.

Mradi huu unalenga kukuza mimea inayostahimili ukame, uchimbuzi kidogo wa udongo, kuhakikisha kuwepo kwa funiko la udongo wakati wote, upanzi wa mimea mbadala kila msimu, upanzi wa mimea na kulima kwekwe kwa wakati ufaao, na uboreshaji wa uhifadhi wa vyakula. Mimea ambayo inakuzwa kwa sasa ni mihogo, pojo na mtama.



Shamba la Majaribio katika Wadi ya Kikoneni, Kaunti Ndogo ya Lunga Lunga.



Mkulima Jairo Ritho akitayarisha shamba kutumia jembe la kuvutwa na ngombe, katika Wadi ya Kikoneni, Kaunti Ndogo ya Lunga Lunga.



**Mama Mariam, Mtoa Huduma ya Upanzi, Wadi ya Vanga, Kaunti Ndogo ya Lunga Lunga, akipanda kutumia 'Jab Planter'.**

Mradi umeweza kuwapa mafundisho Walimu Wakuu wa Wakulima 9, Walimu wa Wakulima 173, wakulima 6560 kutoka vikundi 328, na kutengeneza mashamba 328 ya majaribio katika Kaunti yote ya Kwale.

Vikundi vyenye mashamba ya majaribio walifadhiliwa na mbegu, mbolea ya dukani, vifaa vya kupanda, vifaa vya kulima, vifaa vya kulima kwekwe na vipanzi. Wakulima 17 pia walipata vipanzi vya kuvutwa na ngombe. Kila kipanzi kina uwezo wa kupanda eka 5 kwa siku.

Kufikia sasa, wakulima 3464 wameweza kulima heka 2178 chini ya kilimo hifadhi. Mradi umewasaidia zaidi kwa kuwapa mafunzo watoa huduma mbalimbali. Kuna watoa huduma 186 wa kunyunyiza dawa na watoa huduma 20 wa kulima na kupanda. Ili kuhakikisha usalama wa vyakula, watoa huduma 20 kutoka Idara za Afya, Maafisa wa Kilimo Nyanjani na baadhi ya wakulima walifunzwa kuchunguza aflatoxini.

## James Kieti, Mkulima na Mtoa Huduma wa Mradi

Mkulima James Kieti ana shamba la eka 4 katika Wadi ya Kikoneni. Eneo hili ni kati ya maeneo kame ya Kaunti Ndogo ya Lunga Lunga. James ni fundi wa majembe, lakini wakati mradi ulipoanza aliongeza kilimo kama chumo riziki mbadala.



**Bw. James Kieti katika karakana yake.**

James pia ni mtoa huduma za kupanda na amekuwa akisaidia wakulima kwa kutengeneza majembe ya kulima kwekwe.

James amekumbatia kilimo hifadhi kikamilifu. Yeye hutumia dawa kuondoa kwekwe na jembe lisilo chimba udongo kiasi kikubwa wakati wa kutayarisha udongo. Kwa kupanda pojo, James hutumia kifaa cha 'Jab Planter' maalum kwa kupanda ndani ya mitaro na kipalilia kwekwe juujuu ambacho alikitengeneza mwenyewe.

James hulima mahindi eka moja, pojo eka moja, eka moja yenye mchanganyiko wa pojo na mahindi, na eka moja ya kunde.

James ameona mabadiliko katika mavuno shambani kwa kutumia kilimo hofadhi. Mavuno ya mahindi yameongezeka kutoka gunia 4 hadi 12 kwa eka, na gharama ya kukuza ikapungua kutoka Kshs. 10,000 hadi Kshs. 4,000 kwa eka. Pojo pia zimeongezeka kutoka gunia moja hadi tatu kwa eka na gharama ya kukuza ikapungua kutoka Kshs. 9,000 hadi Kshs. 4,500 kwa eka.

Mapato ya mahindi yameongezeka kutoka Kshs. 45,000 hadi Kshs. 110,000, ya pojo kutoka Kshs. 40,000 hadi Kshs. 120,000, na kunde kutoka Kshs. 20,000 hadi Kshs. 90,000. Pia, ameuza majembe ya kupalilia kwekwe 25 kwa Kshs. 300 kila moja. Haya ni mapato tangu mradi uanze.

Mafanikio haya yamemuezesha kusomesha watoto wake, kuboresha nyumba yake na kupanua biashara yake ya ufundi wa kuchomelea na kutengeneza majembe.



**Bw. John Safari (Muandishi wa Makala) ni Mkurugenzi Mdogo wa Kilimo, na Msaidizi wa Nyanjani, Shirika la Chakula Duniani, Kaunti ya Kwale.**



# Rasilimali Bahari

## Rasilimali Muhimu Barani Afrika inayoweza kutimiza ndoto ya 'Africa Tunayoitaka'

Bara Afrika ina utajiri mkubwa ki-rasilimali, kijamii na kitamaduni. Kati ya rasilimali kubwa Afrika ambayo haijatumika kikamilifu ni rasilimali bahari. Kati ya nchi 54 za Afrika, 38 zina fuo ya bahari ya pwani.

Afrika ina takriban kilomita milioni 13 mraba za eno la bahari ikijumuisha maeneo ya kiuchumi ya bahari, takriban kilomita milioni 6.5 mraba za sakafu ya bahari, na takriban kilomita 240,000 mraba za maeneo ya ziwa. Kwa jumla, bara Afrika lina rasilimali kubwa ya bahari ambayo, ikitumiwa kikamilifu, inaweza kuchangia meandeleo endelevu kwa nchi za Afrika.

Matumizi endelevu, usimamizi na uhifadhi wa rasilimali na mazingira ya bahari na rasilimali zinazohusiana na rasilimali hii, ndio inafahamika kama uchumi wa bahari. Inajumuisha sekta nyingi kama vile uvuvi, utalii, usafiri, ujenzi wa meli, kawi, uvumbuzi wa chembechembe hai za kutengeneza dawa na bidhaa nyingine, uchimba madini chini ya bahari na shughuli husika nyinginezo.

Mfumo wa uchumi wa bahari unasisitiza uhusiano bora wa sekta ambazo, kwa ujumla, zinatoa huduma kutokana na kuvuna kwa viumbe hai na visivyo hai, na kufaidi nchi zenye pwani, nchi visiwa na nchi zisizo na pwani. Uchumi endelevu wa bahari pia inachangia mambo muhimu ya kijamii kama vile usawa wa jinsia, kujitosheleza kwa chakula na maji, kupunguza umaskini, uhifadhi wa utajiri, na ubunifu wa nafasi za kazi.

6 Umuhimu wa uchumi wa bahari umetambuliwa na Umoja wa Mataifa kwa kupitisha Malengo ya Maendeleo Endelevu na hasa Lengo la 14 kuhusu uhifadhi na matumizi endelevu ya bahari na rasilimali zake. Umoja wa Afrika pia umetambua uchumi wa bahari kama moja ya nguzo za Agenda 2063 kuhusu Afrika Tunayoitaka.

Rasilimali hai zinazopatikana katika bahari ya Afrika inawezesha Afrika kuongeza uvuvi na kilimo cha maji kwa minajili ya kukuza viwanda vya dawa, kemikali na vipodozi. Ukuzaji wa viwanda kutumia rasilimali unahitaji rasilimali hai pamoja na vilengecho vingine kama vile madini na uvumbuzi wa rasilimali mpya ya kawi. Kwa hivyo, Afrika iko katikati ya biashara duniani, hasa biashara ya kuongeza ubora bidhaa.

Manufaa ya rasilimali hizi zitapatikana kwa urahisi na haraka ikiwa Afrika itatumia teknolojia inayofaa, ijapo Afrika iko nyuma kiteknolojia. Soko la teknolojia hai inatarajiwa kufika bilioni 5.9 za Marekani kufikia 2022. Mchango mkubwa unatazamiwa kutoka kwa uwekezaji katika utafiti wa teknolojia hai ya bahari na soko linalokuwa la viungo asili vya bahari. Teknolojia hai ni muhimu kwa kutengeneza vyakula vipya, utengenezaji madawa na vipodozi.

Mbali na viumbe hai, rasilimali ya bahari pia ina uwezo mkubwa wa kuzalisha kawi endelevu. Shirika la Kimataifa la Kawi linakisia kuwa bahari ina uwezo wa kutoa kawi endelevu mara nne ya mahitaji ya sasa ya kawi ulimwenguni. Kwa sasa, takriban asili mia 30 ya mafuta na gesi duniani inatoka baharini na inatazamiwa kuendelea kukimu mahitaji ya kawi ulimwenguni hadi pale tutakapoanza kutumia uwezo wa bahari kutoa kawi endelevu.

Afrika, ijapo ina rasilimali nyingi, ina athirika kutokana na janga la umaskini, ikiwa asili mia 46 ya wakazi wake wako katika umaskini mkubwa. Umoja wa Afrika umefanya bidii ya kuwahamasisha wanachama wake kuhusu umuhimu wa uchumi wa baharini, hasa katika kukuza utajiri na kupunguza janga la umaskini. Kwa kusisitiza umuhimu huu, Umoja wa Afrika uliunda Mkakati wa Pamoja wa Bahari, na kuweka uchumi baharini kama nguzo muhimu ya Agenda 2063 ya Afrika Tunayoitaka. Umoja wa Afrika pia ulianzisha Siku ya Mwafrika, Julai 25 na Mwongo wa Bahari (2015-2025) ili kuhamasisha mipango na kazi kuhusu uchumi wa baharini.

Kufikia sasa, nchi nyingi Afrika zimeanza kutambua umuhimu wa uchumi wa bahari. Baadhi ya nchi za Afrika zimeanza kuunda sera, mikakati na miongozo ya uchumi wa bahari kama vile Mauritius na Ushelisheli.

Kuna changamoto ambazo zinazuia kupatikana kwa manufaa ya uchumi wa bahari. Changamoto hizi ni kama vile hatari za mabadiliko ya hali ya hewa, ukosefu wa usalama baharini, tsunami na vimbunga, ongezeko la maji baharini, ongezeko la asidi baharini, uvuvi wa kupita kiasi kutokana na uvuvi haramu na matumizi ya mbinu zisizo endelevu za uvuvi, uchafuzi na uharibifu wa maeneo ya bahari.

Chanagamoto nyingine ni kama vile ukosefu wa njia za kufikia rasilimali zinazo milikiwa kwa pamoja. Vilevile, teknolojia muafaka na uzoefu unaohitajika kufaidi uchumi wa bahari, imekuwa kizuizi. Malengo yasiyo sawia baina ya nchi inaweza kupunguza uwezo wa nchi kushirikiana na hata kuleta hofu kati yao

Uwezo wa Afrika kunufaika na uchumi wa bahari utategemea pa kubwa jinsi Afrika itakavyo jifafanulia swala zima la maendeleo na ufanisi, kwa kukuza fikra bunifu. Kwa kuongezea, kuna haja ya kujumuisha vikundi vyote vya kijamii, hasa wanawake, vijana, jamii mashinani na jamii zilizo tengwa, na kutambua nafasi za kipekee ambazo wadau hawa wanaweza kuchangia ili kuleta maendeleo ya haraka.

Katika mchakato mzima, kuna umuhimu wa kulinda tamaduni zetu za Afrika. Maelfu ya jamii asili wanaendelea kutumia tamaduni na njia zao asili za chumo riziki. Chumo riziki hizi sio tu njia za kujipatia mapato, bali pia inawakilisha kitambulisho chao.



***Bw. Moses Ziro (Muandishi wa Makala) ni Katibu wa Watu Mazingira Ulimwenguni, na Mkurugenzi Mtendaji wa Africa Nature Organization.***



# BUSTANI ZA MATUMBAWE

## *Mbinu Mpya ya Kuboresha Mazingira ya Bahari*

Bahari na rasilimali zake daima hushangaza. Ina aminika kuwa hatujavumbua siri nyingi ambazo bahari imeficha ukilinganisha na kile tunajua kuhusu rasilimaki za nchi kavu. Lakini kuna jambo moja ambalo sote tunalifahamu vyema. Kwamba bin Adam wameendelea kuharibu bahari kwa kiasi kikubwa mno kwa uchafuzi, hasa uchafuzi wa plastiki na umwagikaji wa mafuta baharini.

Hata ingawa bahari zetu si safi, zimeenedelea kuzalisha bidhaa na huduma ambazo zimesaidia maisha katika dunia. Ukamilifu na uzalishaji wa bahari umepigwa jeki na uvumbuzi wa mbinu mpya ya kurudisha upya maeneo ya bahari ambayo yameharibika kupitia upanzi wa matumbawe.

Jamii ya kisiwa cha Wasini ni miongoni mwa jamii za kwanza Afrika kufanya majaribio na kufaulu kupanda matumbawe. Majaribio haya yalitumia ujuzi asili na wa kisayansi kupanda vipande vya matumbawe katika kitalu (nasari) kabla kuhamisha katika sehemu zilizoharibika za bahari. Jamii ilisaidiwa na shirika la Africa Nature Organization, Shirika la Utafiti wa Bahari na Uvuvi Kenya na Idara ya Uvuvi.

Ina julikana kuwa sehemu za matumbawe ni sehemu muhimu za makao kwa aina nyingi za viumbe hai baharini. Zinatambulika kwa kutoa manufaa mengi ya kiuchumi, ki-ekolojia, urembo na tamaduni. Sehemu hizi pia ni muhimu kama mazalio na maficho ya samaki na viumbe hai vya baharini.



Matumbawe yaliyo tayari kupandwa.

Kutokana na uharibifu wa maeneo ya bahari na bin Adam kupitia uchafuzi, uvuvi usio endelevu na athari za mabadiliko ya hali ya hewa, matumbawe yana zidi kupotea. Hii ni kwa sababu, matumbawe haya wezi ongezeko la joto baharini, asidi baharini, mawimbi, miale mikali ya jua na mrundiko wa mchanga. Uharibifu huu unachoma, kuua, kupunguza uwezo wa kuzaa na hata kuhatarisha matumbawe na magonjwa.

Mchakato wa kutengeneza bustani ya matumbawe huanza kwa kukuza vipande vya matumbawe katika kitalu ili kuyakinga na athari zinazokumba matumbawe yakiwa madogo. Baada ya kukuzwa katika kitalu, matumbawe yaliyokomaa hupandwa katika sehemu zilizo chaguliwa kwa minajili ya kuziregesha upya. Kwa sasa, utengenezaji bustani za matumbawe unatumiwa kama chombo cha kuregesha matumbawe sehemu zilizoharibiwa.

Kuna hatua 10 zilizotumiwa na jamii ya Wasini kutengeneza bustani za matumbawe. Nazo ni: -

1. Kuhamasisha jamii kuhusu umuhimu wa kuregesha upya sehemu zilizoharibika za matumbawe,
2. Kutambua sehemu zilizoharibika za matumbawe kupitia ushirikiano wa jamii na wataalam, na kutoa ramani, kuzitenga sehemu hizi na kuorodhesha kazi za kipaumbele,



Ufuatilizaji wa ukuaji wa matumbawe

3. Kufanya utafiti wa msingi kwa maeneo yaliyo lengwa kwa kukusanya habari kama vile wingi wa samaki, aina za samaki, shughuli za uvuvi na utalii, na kadhalika,
4. Kutambua aina za matumbawe na sehemu za kutoa mbegu za matumbawe,
5. Mafundisho kwa jamii na wadau wengine kuhusu mchakato wa kutengeneza bustani za matumbawe,
6. Baada ya mafundisho, sehemu za kuweka vitaru zilichaguliwa na kutengezwa kutumia matofali,
7. Mbegu za matumbawe zilikusanywa na kupandwa katika vitalu,
8. Kufuatizia ukuaji wa matumbawe katika kitalu na kuhakikisha usafi ili kuongeza ukuwaji haraka wa matumbawe,
9. Matumbawe yaliyo komaa katika kitalu yapandwa katika sehemu zilizo tengwa kwa upanzi wa matumbawe,
10. Kufuatizia mara kwa mara ukuaji wa matumbawe katika bustani.

Kwa sasa, kuna ongezeko la manufaa kutokana na wingi wa samaki na watalii wanaotembelea bustani za matumbawe. Watalii wanatoka taasisi za elimu, watafiti na vikundi vya kijamii wenye hamu ya kuanzisha bustani zao.

Kuna mpango wa kupanua bustani za matumbawe katika kisiwa cha Wasini na sehemu nyinginezo katika pwani ya Kenya.



Bw. Abdalla Omar Juma (Muandishi wa Makala) ni Katibu wa Wasini Beach Management Unit, kikundi cha kijamii kilichoundwa kufuatia sheria ya Usimamizi na Uendelezaji Uvuvi Kenya.

# MSITU WA MADUNGUNI

## Msitu Asili Wa Pwani Ya Kenya Unaoangamia Polepole



***Bw. Raphael Ngumbao, Mwenyekiti wa Friends of Madunguni Forest, akiwa juu ya poromoko la Madunguni. Maporomoko zaidi yanaonekana kwa upande wa nyuma ya picha.***

Msitu wa Madunguni ni msitu wa serikali wenye eneo la heka 951.85. Msitu huu ni moja wa misitu asili ya sehemu kame za pwani.  Unapatikana kaskazini mashariki mwa msitu mashuhuri wa Arabuko Sokoke. Barabara ya Malindi-Sala Gate inagawanya misitu hii miwili.

Msitu wa Madunguni, ni hifadhi ya wanyama na miti asili inayopatikana tu katika eneo hili la Madunguni-Arabuko Sokoke. Ni masilikitiko kuwa msitu wa Madunguni umeendelea kuzorota kutokana na uvamizi wa maskwota, watengeza makaa, wavuna mbao na wanao tafuta kuni za kuuza.

Ina kadiriwa kuwa asili mia 75 ya msitu umepotea tangu miaka ya 1980 kwa sababu ya uvamizi huu. Madhara yake yamekuwa mmomonyoko wa udongo unao athiri mashamba na makazi sehemu za chini ya Madunguni. Mmomonyoko huu umeleta maporomoko makubwa sehemu kadhaa za msitu.



***Dungu***

Msitu wa Madunguni ulipata jina lake kutoka kwa kijiji cha Madunguni, kinacho julikana kwa mashamba yaliyo na rotuba na sehemu muhimu ya kuzalisha chakula kwa Kaunti ya Kilifi. Dungu, ambapo wingi wake ni madungu, ni nyumba iliyo inuliwa kwa miti ili kukinga wakulima dhidi ya uvamizi wa simba na wanyama wengine wa pori.

Msitu wa Madunguni awali ulikuwa chini ya usimamizi wa Serikali za Wilaya. Na kwa wenyeji wa Madunguni waliuhifadhi kwa sababu ya kupata kuni kwa vile hawakuwa na ruhusa ya kuingia katika msitu wa Serikali wa Arabuko Sokoke. Lakini muhimu zaidi ni kwamba, wenyeji walitumia msitu huu kutabiri mvua na hali ya hewa. Na kwa hivyo, palikuwa sehemu takatifu kwa wenyeji.

Lakini mambo yalianza kubadilika kuanzia 1969. Wakaazi wa eneo la Maili 10 ya pwani, ikijulikana wakati huo kama Mikaoni, walianza kuvamia msitu wakitafuta kuni, mbao, kulima na hata kutengeneza makaaa. Sehemu ya Mikaoni ilijumuisha vijiji vya Kakuyuni, Mere na Mida.

Mnamo 1971, jamii ya Madunguni pamoja na Afisa wa Misitu, Bw. Tinga, waliarifu Serikali ya Mkoa kuhusu uharibifu huu. Machifu Awadh na Athmani Ndurya, wa sehemu ya Mikaoni, walipewa jukumu la kusitisha uharibifu huu kutoka kwa wakaazi wanaotoka sehemu zao.

Kutokana na ushirikiano wa Afisa wa Misitu na jamii ya Madunguni, kijiji cha Madunguni waliweza kuunda Kamati ya Mazingira ya Madunguni.

Mwaka huu pia Idara ya Misitu ilinuia kujenga kituo kidogo cha utafiti eneo la Arabuko Sokoke ndani ya Msitu wa Madunguni. Lakini wenyeji wa Madunguni wakiongozwa na mwenyekiti wa Kamati ya Mazingira ya Madunguni, Bw. Ngumbao Mwanzili, hawa kukubaliana na wazo hilo. Wangekubali, pengine msitu wa Madunguni ungebadilishwa kuwa wa Serikali.

Kufikia 1980, uharibifu wa msitu ulikuwa umekithiri. Bw. Ngumbao Mwanzili alipata kuungwa mkono na Bw. Kaingu Bindurya na Abdalla Ndema, wakereketwa waliosaidia kuhamasisha jamii kuhusu uharibifu wa msitu. Kwa juhudi zao, wavamizi walifurushwa na Serikali ya Mkoa na kujipatia makao karibu na msitu. Kufikia 1987, wavamizi walirudi tena kufanya makao na kuendelea kulima ndani ya msitu.

Idadi ya wavamizi iliendelea kuongezeka hadi 500 mwaka wa 1996. Wanasiasa pia wakaingilia swala la msitu wa Madunguni na kuwapa moyo wavamizi kuendelea kulima. Hali ilibadilika wakati wavamizi wa zamani na wapya walipoanza kuteta wenyewe kwa wenyewe. Wengine walipoteza maisha yao katika vita hivyo.




***Sehemu kubwa ya msitu imefyekwa na kufanywa makao na mashamba***




Serikali ya Mkoa ilishindwa kukabiliana na mwingilio wa wanasiasa katika kutatua mzozo wa msitu. Hatimaye, iliwabidi kuwafurusha wavamizi badala ya kuwapeleka kortini ambako wanasiasa walisaidia kurushwa kwa kesi zao.

Vijana wa Madunguni pia hawa kuachwa nyuma katika harakati za kuokoa msitu wao. Mnamo 2001, vijana waliunda na kusajili Friends of Madunguni Forest, kama njia moja ya kusaidia juhudi za Kamati ya Mazingira ya Madunguni. Mwaka 2004, pamoja na wadau wengine waliweza kumshawishi Mbunge wa Malindi, Bw. Abubakar Badawy kupeleka mswada bunge wa kubadilisha msitu huo kuwa wa Serikali. Na ombi hilo likapitishwa.




Wavamizi nao hawa kuachwa nyuma. Waliweza kupeleka kesi kortini kupinga kuorodheshwa kwa msitu kuwa wa Serikali. Korti iliamuru wavamizi wabaki bila kufanya shughuli zozote ndani ya msitu hadi kesi itakapo amuliwa. Kesi bado haija amuliwa.

Kwa muda huu, msitu umeendelea kuharibiwa bila kujali amri ya Korti. Ukulima, utengenezaji makaa, na ujenzi wa shule, makanisa na msikiti zimeendelea ndani ya msitu. Idadi ya wavamizi pia imezidi kuongezeka hadi takriban watu 2000, na wana amini kuwa siku moja Serikali itachoka na kuwaachia msitu.

Kulingana na shughuli zote zinazo endelea ndani ya msitu, inakadiriwa kuwa msitu wa Madunguni utaangamia chini ya miaka 5. Athari kubwa zaidi haitakuwa tu kwa msitu, bali pia kwa wakaazi wa Madunguni ambao mashamba yao yamepoteza rotuba kutokana na limbikizo la udongo usio rotuba kutoka msituni.

Picha 1, 2 na 3: Wanachama wa mtandao wa Watu Mazingira Ulimwenguni kutoka Madunguni wakipanda miti nani ya msitu wa Madunguni mwaka wa 2017.



Waandishi wa Makala:

Bw. Raphael Ngumbao, Mwenyekiti, Friends of Madunguni Forest, na mwanachama, Watu Mazingira Ulimwenguni.

Bwr. Charles Thoya, Mwenyekiti, Jilore Community Forest Association na mwanachama, Watu Mazingira Ulimwenguni.

Bw. Weston Mure, (Picha 2), mkaazi wa Madunguni na mwanachama, Watu Mazingira Ulimwenguni.

# Watu Mazingira Ulimwenguni
# Kamati Kuu

Silvanus Uunona
Mwenyekiti, Watu Mazingira,
na Mshirikishi,
Jukwaa la Maji
(Namibia).





Yaa Tiwah,
Mwenyekiti Mwenza,
Watu Mazingira,
na Mshirikishi,
Kilimo Hifadhi na Uvuvi,
(Ghana)



Frank Maro,
Mweka Hazina, Watu Mazingira,
na Mshirikishi, Jukwaa la
Biashara Mazingira
(Tanzania).



Phathisani Tabengwa,
Mshirikishi, Jukwaa la Elimu
Mazingira na Hamasisho,
(Zimbabwe).



Emma Musingo
Mshirikishi, Jukwaa la Jamii
Asili,
(U.ganda).



Nancy Saumu
Mshirikishi, Jukwaa la Wanyama
Pori na Misitu,
(KENYA).



Cheli Gurung,
Mshirikishi, Jukwaa la Vijana
(NEPAL).



Moses Ziro,
Katibu, Watu Mazingira,
(KENYA).

## Watu Mazingira Ulimwenguni

# Washirikishi Wenza



Michael Kusundwa,
Jukwaa la Jamii Asili,
(TANZANIA)



Dorothy Syallow,
Jukwaa la Wanyama Pori na Misitu,
(KENYA)



Raymond Mwambire,
Jukwaa la Vijana,
(KENYA)

Soledad Castro,
Jukwaa la Maji,
(COSTA RICA)





Fadhila Ghikas,
Jukwaa la
Biashara
Mazingira,
(KENYA)



Gaston Setondji,
Jukwaa la Kilimo Hifadhi na
Uvuvi,.
(BENIN)



Zelalem Abera
Jukwaa la Elimu Mazingira na
Hamasisho
(Ethioia)

# Karibuni Nyumbani!

Mtandao wetu wa Watu Mazingira Ulimwenguni umeweza kukuwa kwa haraka na sasa tuna wanachama 424 wakiwakilisha nchi 16 duniani. Nchi hizi ni ni Bangladesh, Benin, Cameroon, Costa Rica, Ethiopia, Ghana, Kenya, Malagasi, Marekani, Msumbiji, Namibia, Nepali, Tanzania, Uganda, UJapani, na Zimbabwe.

Mwaka huu (2018), wanachama 36 walisajiliwa kutoka Cameroon (2), Bangladeshi (1), Kenya (27), Malagasi (2), Msumbiji (1) na Nepali (3). 7 kati yao walisajiliwa robo ya nne ya 2018. Mwaka 2018, tuliweza kusajili vijana 5, chini ya miaka 21.



Paul, KENYA



Ram, NEPAL



Sandra, KENYA



Bambo, KENYA



Cynthia, KENYA

# Wasiliana Nasi!

Daima tuna furaha kusikia na kusoma kutoka kwako. Ikiwa una swali ama maoni ya vile tunaweza boresha mtandao wetu ama jarida letu, usisite kuwasiliana nasi.

Tunakaribisha makala amabayo tunayachapisha katika Jarida letu la Watu Mazingira Ulimwenguni. Unaweza kuangazia maoni yako kuhusu mazingira, ukatoa ripoti kuhusu mradi wako nyumbani, warsha uliyohudhuria ama shughuli yoyote ile ya kimazingira.

Wasiliana nasi kupitia viunganishi vifuatvyo: -

people4nature@africanature.or.ke

+254 717 127 800


People4Nature Global

People4Nature

People4Nature Global

People4Nature Global

www.africanature.or.ke



# Watu Mazingira

## Ulimwenguni!

People4Nature Belong!


S.L.P 2227, 80100, Mombasa Kenya

Simu 1: +254 717 127 800

Simu 2: +254 780 127 800

Hazina Mazingira: +254 777 127 800